E. Sampuli za hati kwa wakulima wadogo na wale wanaonnua moja kwa moja kutoka kwao

Sampuli hizi nne za hati zinajumuisha:

- Sampuli ya mkataba kutoka kwa wakulima wadogo hadi kwa mnunuzi
- Orodha iliyopendekezwa ya rekodi ambazo wakulima wadogo na wanunuzi; wanapaswa kuhifadhi
- Muundo wa uhifadhi wa rekodi
- Orodha ya ukaguzi wa hatua za kiafya na kiusalama zilizochaguliwa.

Hati hizi zimenakiliwa kwa ruhusa ya: Natural Resources Institute Uk[2],

E. 1 Sampuli ya mkataba baina ya mkulima na kampuni kwa ukuzaji wa maharagwe mabichi

1 Kwa jumla:

1. Wakulima wa kijiji cha .....(wakulima hawa) wangependa kukuza maharagwe mabichi na kampuni .....(kampuni hiyo) pia ingependa kuwasaidia na kununua mazao yao na kuyauza ng'ambo.
2. Mkataba huu unaeleza mapatano na masharti ya kazi ambayo kwayo wakulima watakuza maharagwe mabichi, nayo kampuni itawasaidia, itanunua na, itayatengeneza na kuyauza.

2 Kampuni inakubali:

1. Kupima na kukadiria kufaa kwa ploti inayopendekezwa na wakulima hao kwa ukuzaji wa maharagwe mabichi.
2. Kutoa mbegu za hali ya juu kwa mkulima wakati mzuri wa upanzi na kiasi kinachohitajika kupanda eneo la ardhi lililokubaliwa.
3. Kutoa kwa malipo ya pesa taslimu (au kwa mkopo punde tu mkulima amekuwa imara na wa kuaminika) aina na kiasi cha mbolea na kemikali za kilimo zinazohitajika kwa eneo lililopandwa maharagwe mabichi na mkulima.
4. Kuwashauri wakulima kuhusu vipengele vyote vya kiufundi vya ukuzaji wa maharagwe mabichi.
5. Kununua maharagwe mabichi yote yenye ubora unaokubalika yaliyokuzwa na wakulima hao kwa bei iliyotangazwa hapo mwanzoni mwa kila msimu wa upanzi. Masharti ya ubora yataelezwa katika ratiba 1.
6. Kulipa mkulima malipo yake kama yaliyoelezewa kwenye aya ya 4 hapo chini.

3 Mkulima anakubali:

1. Kutumia sehemu ya shamba lake lililochunguzwa na kukubaliwa na kampuni kwa ajili ya ukuzaji wa maharagwe mabichi katika kipindi cha mkataba huu.
2. Kupanda mbegu za maharagwe zilizotolewa na kampuni kwenye shamba hili na tarehe kamili pamoja na kufuata taratibu zilizopendekezwa na kampuni.
3. Kufuata mashauri yote ya kiufundi yaliyotolewa na kampuni kuhusu kupanda, kunyunyuzia maji, kupalilia, kuweka mbolea, kudhibiti wadudu na magonjwa, kuvuna, kuchagua na kufunga katika vifurushi maharagwe mabichi.
4. Kuuza maharagwe mabichi yote yenye ubora unaokubalika yaliyokuzwa kwenye shamba kwa kampuni kwa bei

2. *Smallholders in Export Horticulture: a Guide to Best Practices*, The University of Greenwich, 2002.

na utaratibu ulioelezewa katika aya ya 4 hapo chini.

5. Kuwa mwanachama wa kikundi cha wakulima wa …… na kuchangia katika kutengeneza nyenzo za watu wote za kunyunyuzia maji, kusambaza pembejeo, kuchagua, kufunga zao katika vifurushi n.k kama ilivyokubaliwa na kikundi.

4 Malipo ya maharagwe mabichi na pembejeo za uzalishaji yataamuliwa kama ifuatavyo:

1. Bei ya chini ya kunulia kila gredi ya maharagwe mabichi itatangazwa na kampuni angalau mwezi mmoja kabla ya mwanzo wa kila msimu wa upanzi.
2. Bei za kuuzia mbolea na kemikali za kilimo zitatangazwa wakati huohuo lakini zinaweza kubadilika mwaka unapoendelea kulingana na pandashuka za kima cha mabadilishano ya fedha.
3. Malipo ya maharagwe mabichi yanayowasilishwa kila mwezi, baada ya kuondoa gharama ya mbolea na kemikali za kilimo zilizochukuliwa kwa mkopo, yatafanywa kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata.

5 Adhabu na malipo ya ziada (bonasi):

1. Ikiwa mkulima amewasilisha maharagwe mabichi yasiyotimiza viwango vya ubora vilivyokubaliwa, kampuni itayakataa. Mkulima anaweza kuyawasilisha tena baada ya kuyachagua, lakini kampuni hailazimishwi kupokea maharagwe ambayo hayatimizi viwango vya ubora vilivyokubaliwa.
2. Ikiwa mkulima ameshindwa kufuata taratibu zilizoelezewa katika mkataba huu, basi ataonywa kwa maneno na kwa maandishi. Baada ya maonyo matatu kwa maandishi, kampuni itakuwa na haki ya kusimamisha mkataba huo.
3. Ikiwa kampuni imeshindwa kutimiza majukumu yake kama yalivyoelezewa katika aya ya 2 hapo juu, mkulima ana haki ya kudai fidia ya thamani ya huduma zilizoachwa au ya thamani ya zao lililopotea, kwa vima vilivyokubaliwa baina ya kampuni na kikundi cha wakulima.
4. Ikiwa mkulima amewasilisha maharagwe mabichi ambayo yamepitisha viwango vya ubora vinavyotakiwa au kiasi kilichotarajiwa cha uzalishaji, atastahili malipo ya ziada kwa kiasi kilichokubaliwa baina ya kampuni na kikundi cha wakulima.

6 Muda wa mkataba:

1. Mkataba huu utadumu kwa msimu mmoja wa ukaguzaji kuanzia tarehe ya kuutia sahihi hadi mwisho wa mavuno yenye kufidia gharama ya zao la maharagwe mabichi.
2. Ikiwa pande zote zimeridhika na matokeo ya mkataba, mkataba huo unaweza kurudiwa tena kwa msimu wa baadaye lakini pande zote hazilazimiki kurudia tena mkataba huo.

7 Suluhisho la mizozo:

1. Mzozo wowote unaotokana na mkataba huu utasuluhishwa, inapowezekana, kupitia mazungumzo baina ya kampuni, kikundi cha wakulima na mkulima.
2. Mzozo wowote usioweza kusuluhishwa kwa utaratibu huu utapelekwa kwa msuluhishi anayekubalika na pande zote zinazohusika.

8 Sahihi:

Nimesoma na kuelewa yaliyomo kwenye mkataba huu na ninatia sahihi kwa hiari yangu mwenyewe.

_____ (mkulima)
_____ (kampuni)
_____ (shahidi)
_____ (tarehe)

RATIBA YA 1: MASHARTI YA GREDI NA UBORA WA MAHARAGWE MABICHI.

1. Uonyeshaji halisi wa gredi

1. Maharagwe ya gredi ya 1 (nzuri zaidi) yana urefu wa kutoka 6.5cm hadi 9.5cm.
2. Maharagwe ya gredi ya 2 (nzuri) yana urefu wa kutoka 9.5cm hadi 11.0cm.
3. Saizi nyingine hazitakubaliwa.

2. Masharti ya ubora: Maharagwe yatakayokubaliwa lazima yawe:

1. Hayana wadudu, michubuko, kovu, vilio;
2. Hayana matope, vumbi au vifusi vinginevyo;
3. Hayajavunjika au kuharibiwa kwa njia yo yote ile;
4. Hayajakunjwa;
5. Yamevunwa na mabaki ya kalisi;
6. Mabichi na yasinyaushwe na jua au vitoa joto vinginevyo;
7. Ni ya rangi ya kibichi ya asilia, isiyo na madoadoa kutokana na ugonjwa, moshi, n.k.

Rejeo: *Linking Farmers to Markets: an Operational Manual, FAIDA, Arusha*, inayokuja mwaka wa 2005.

E.2 Rekodi za kuhifadhiwa na wakulima wadogo, walanguzi na makampuni wanunuzi

Rekodi za wakulima wadogo	Rekodi za walanguzi	Rekodi za makampun
• Shughuli za nyanjani tarehe, masaa ya kazi, pembejeo zilizotumika, matatizo yaliyowakumba. • Gharama za kila kazi (wafanya kazi na pembejeo zilizonunuliwa) • Mikopo iliyochukuliwa tarehe, mkopaji, masharti na malengo yake. • Kiasi na ubora wa bidhaa zilizovunwa, kuuzwa, kukataliwa, kutumiwa. • Thamani ya jumla ya mauzo ikiwa ni pamoja na malipo ya ziada au malipo ya adhabu. • Mikopo iliyolipwa na iliyosalia. • Makadirio yake ya utendaji na mafanikio.	• Huduma zilizotolewa kwa wakulima wadogo na kampuni. • Malipo yaliyotozwa, gharama halisi, chanzo cha fedha kwa gharama ambazo hazijakamilika kulipwa. • Makadirio yake binafsi matokeo ya huduma zilizotolewa, mawazo ya uboreshaji unaowezekama.	• Idadi ya wakulima, eneo, lokesheni, na aina ya zao • Eneo la upanzi ya mukulima mdogo na lokesheni • Idada, aina na gharama ya mbegu na pembejeo zingine zilizosambazwa • Aina na gharama ya huduma zingine zilizotolewa • Mikopo zilizotolewa na iliyolipwa • Idadi, masharti na gharama ya zao lililouzwa • Gharama ya utengenezaji, usafirishaji, ukusanyaji na uuzaji wa bidhaa • Makadirio yake ya utendaji na mafanikio.

E.3 Sampuli ya muundo wa kusimamia na kuweka rekodi kwa wakulima wadogo

1 Mkulima

a. Jina……
b. Anwani…

2 Eneo

a. Lokesheni
b. Mwinuko
c. Topografia
d. Aina ya mchanga
e. Mvua: wastani ya mwaka (mm)
f. Mvua wastani ya mwezi (mm)
g. Halijoto: ya juu kabisa ya mwezi…
h. Halijoto ya chini kabisa ya mwezi…….
i. Ugavi wa maji ya unyunyiziaji (chanzo, ubora, tegemeo)
j. Mimea
k. Matumizi ya ardhi hapo awali

3 Kipimo cha eneo la zao

a. Eneo zima la shamba (ha)
b. Eneo la upanzi la mwaka huu (ha)
c. Eneo la upanzi la mwaka jana (ha)mazao (kg)

4 Matayarisho ya shamba

Tarehe	Kazi	Mbinu	Gharama	Matokeo

5 Shughuli za kitalu cha miche (ambapo miche inatolewa kwa ajili ya kupandikiza)

Tarehe	Kazi	Vifaa vilivyotumika (aina, kiasi, gharama)	Wafanya kazi (idadi na gharama)	Matokeo

6 Kupandikiza (inapotumika)

Tarehe	Eneo lililopandwa	Idadi ya miche	Nafasi baina ya mistari	Gharama	Matokeo

7 Upanzi wa mbegu moja kwa moja (inapotumika)

Tarehe	Eneo	Mbegu (gm)	Mbinu	Nafasi baina ya mistari	Gharama	Matokeo

8 Matumizi ya mbolea

Tarehe	Eneo	Kiasi (gm)	Aina	Gharama ya vifaa	Gharama ya wafanya kazi	Athari

9 Unyunyiziaji maji.

Tarehe	Eneo lililonyunyuziwa	Mbinu	Kiasi / gharama ya vifaa	Idadi / gharama ya wafanya kazi	Matokeo

10 Uzuiaji wa magugu

Tarehe	Eneo lililopaliliwa	Mbinu	Kiasi / gharama ya vifaa	Idadi / gharama ya wafanya kazi	Matokeo

11 Uzuiaji wa wadudu na magonjwa

Tarehe	Aina ya mdudu / ugonjwa	Matokeo kabla ya dawa	Kiasi / gharama ya vifaa	Idadi / gharama ya wafanya kazi	Matokeo baada ya dawa

12 Mavuno

Tarehe	Eneo	Hali ya zao	Mbinu	Gharama	Matokeo

13 Kuchagua, kusafisha na kufunga mazao katika vifurushi

Tarehe	Mbinu	Idadi/gharama ya vifaa	Idadi/gharama ya wafanya kazi	Matokeo

14 Mazao na mauzo

Eneo lililovunwa	Tarehe ya upanzi	Tarehe ya kuvunwa	Kiasi cha mavuno	Gredi ya ubora (%)	Thamani ya zao lililouzwa

15.Maoni

E.4 Sampuli ya hatua za kiafya na kiusalama zilizochukuliwa.

Kwa vyovyote vile, hii si orodha ya ukaguzi wa masuala ya kiafya na kiusalama katika mashamba madogo. Inashughulikia baadhi ya masuala ambayo wanunuzi wanapaswa kutambua hasa wanapopanga mafunzo kwa wakulima wadogo kuhusu utendaji salama wa kazi. Orodha hii pia inaweza kuwa msingi wa tangazo linaloweza kutandazwa ili wakulima wadogo waweze kuona (kwa mfano katika vituo vyote vya ukusanyaji wa mazao) lakini itahitaji kuandikwa upya kwa hadhira hiyo na hasa ikiwa na vielelezo vyenye mifano ya utendaji:

- Visu na vifaa vingine lazima viwe na makali hii inapunguza hatari ya kujeruhiwa kutokana na matumizi ya nguvu nyingi wakati wa kupuna na kuvuna.
- Ikiwa mashine zinatumiwa, sehemu zinazosongea zinapaswa kufunikwa kila inapowezekana.
- Mafunzo ya kutosha ya kiafya na kiusalama yanapaswa kutolewa ikiwa teknolojia na /au utendaji wa kazi mpya inatumiwa; kwa mfano ikiwa mbolea au viuadudu vimependekezwa, hatua zinapaswa kuchukuliwa za kusaidia wakulima wadogo wasioweza kusoma maagizo.
- Mbolea na viuadudu vilivyopendekezwa vinapaswa kufunganywa katika vifurushi ambavyo wanawake wanaweza kubeba.
- Vyoo havipaswi kuwa karibu na maji yaliyo wazi ya kunyunyizia au kunywa.
- Vyoo vilivyowekwa mahali panapofaa vinapaswa kuwa karibu na maeneo ya uzalishaji hii inawawezesha wakulima wadogo kutumia nyenzo hizi wanapohitaji na kwa hivyo kuzuia matukio ya kwenda haja kubwa shambani, jambo linaloongeza hatari ya uambukizaji wa magonjwa kutokana na vinyesi.
- Wakulima wadogo wanapaswa kupewa mafunzo ya usafi wa kimsingi na wa kibinafsi ili kuzuia uenezaji wa magonjwa kupitia vyakula bila kukusudia (kwa mfano salmonella, shigella, E coli na virusi vya hepatitis A). Wakulima wanapaswa kufahamishwa kuwa usafi bora unawalinda dhidi ya magonjwa.
- Wakulima walio na vidonda vya nje/ngozi; majipu au majeraha yaliyoambukizwa magonjwa katika sehemu za mwili ambazo zinaweza kushikwa na wengine au kuguzwa na mazao mabichi, wasifanye kazi ya kuvuna, kuchagua wala kufunga zao katika vifurushi.